

**CHUO KIKUU CHA KABIANGA**  
**MWAKA WA III MUHULA WA I, 2017/2018**  
**KIS 311: HISTORIA NA MAENDELEO YA KISWAHILI**  
**BEWA KUU NA LA MJINI**  
**MTIHANI MKUU**

**Jibu swali la kwanza na mengine mawili.**

- 1.a) Eleza mchango wa Kiswahili katika kuimarisha maendeleo Afrika Mashariki. (alama 10)
- b) Onyesha namna Wanyarwanda na Wabaganda walivyozuia kuenea kwa Kiswahili katika nchi zao. (alama 10)
- c) Kwa kurejelea runinga moja nchini Kenya, dhihirisha namna kituo hicho cha runinga kinavyokuza Kiswahili. (alama 10)
- 2.a) Huku ukirejelea usanifishaji wa Kiswahili, fafania kwa kina hatua za usanifishaji wa lugha. (alama 8)
- b) Kamati ya Kiswahili Afrika Mashariki iliweka misingi mizuri ya uimarikaji wa Kiswahili siku za baadaye. Jadili. (alama 12)
- 3.a) Eleza umuhimu wa sera kuhusu lugha kwa nchi yoyote. (alama 4)
- b) Ni kwa namna gani sera ya lugha tangu 1981 imechangia kuimarika kwa ujifunzaji wa Kiswahili nchini Kenya? (alama 16)
- 4.a) Fafania mchango wa Mwarabu katika kueneza na kuendeleza Kiswahili Afrika Mashariki. (alama 8)
- b) Bainisha nafasi ya biashara katika ulimwengu wa sasa katika kueneza na kuimarisha Kiswahili. (alama 12)
5. Askofu Edward Steere na Askofu Ludwig Krapf walikuwa na mchango sawia kwa Kiswahili. Tathmini nafasi ya mchango huo katika kustawisha Kiswahili. (alama 20)

*ibig  
shimo - elmu  
E*